



Taarifa kwa Vyombo vya Habari

Watanzania walio wengi hawana habari kuhusu Kodi ya SIM Lakini miongoni mwa wanaojua, wengi hawaikubali

Septemba 11, 2013, Dar es Salaam: Wakati mngurumo wa mjadala kuhusu Kodi ya SIM ukiwa unaendelea, Twaweza ilitumia utafiti wake wa *Sauti za Wananchi*, utafiti unaokusanya takwimu kwa njia ya simu za mkononi, kupima uelewa wa wananchi kuhusu suala hilo na kupata maoni yao.

Matokeo muhimu ya utafiti huu yalikuwa:

Watanzania walio wengi wana fursa ya kutumia simu za mkononi

Ingawa umiliki wa simu za mkononi uko kwa wingi zaidi katika maeneo ya mijini na hasa kwenye kaya tajiri zaidi, robo tatu ya wakazi wa vijijini walionekana wakiishi katika kaya ambazo walau mwanakaya mmoja alikuwa anamiliki simu ya mkononi. Zaidi ya nusu (52%) ya kaya maskini zilionekana kuwa na walau simu moja.

Kiasi cha tozo cha kodi ni sawa na matumizi ya muda wa hewani ya wiki moja katika kaya maskini

Kwa mujibu wa utafiti huu, kwa wastani, kaya maskini zilionekana zaidi kutumia TZS 3,154 kwa mwezi kwa ajili ya matumizi ya muda wa hewani. Hii ina maana kuwa walikuwa wanatumia chini ya kiasi cha tozo ya Kodi ya SIM ya TZS 1,000 kwa wiki. Tofauti na kaya maskini, asilimia 10 za kaya tajiri zilionekana kutumia kwa wastani kiasi cha TZS 45,236 kununua muda wa hewani kila mwezi.

Chini ya nusu ya Watanzania wanafahamu kuhusu Kodi ya SIM

Kitaifa, asilimia 46 tu ya wananchi walioonekana kujua kuhusu Kodi ya SIM. Mijini, watu wengi zaidi (55%) walijua kuhusu kodi hiyo. Uelewa wa wananchi wa vijijini kuhusu kodi hii ilikuwa 41% tu.

Watu wengi hawaikubali Kodi ya SIM

Idadi kubwa zaidi, ya 83% katika makundi yote ya vipato, ilionyesha kutokukubaliana na Kodi ya SIM. Miongoni mwa kaya maskini zaidi 71% haikukubaliana na kodi hii. Upinzani mkali zaidi ulitoka kwenye kaya zilizokuwa na kipato bora zaidi, ambapo 86% ya wananchi wanaipinga kodi hiyo.

Mjadala huu umeibua suala muhimu la kutafakari; Nakisi ya bajeti ya Tanzania ni kubwa na Serikali imedhamiria kuongeza vyanzo vya mapato ya ndani. Kuenea sana kwa simu za mkononi kumezisababishia zionekane kivutio kikubwa cha kupanua wigo wa kodi ya ndani. Hata hivyo, kutokana na tozo ya Kodi ya SIM kuwa sawa kwa wote, inaziumiza zaidi kaya zilizo maskini. Na kwa sababu simu za mkononi na matumizi yake ni vyombo vya nguvu katika ukuaji wa uchumi, je, kuna uwezekano kuwa kodi hiyo ikaleta madhara zaidi kuliko manufaa?

“Vyovyote itakavyokuwa” Rakesh Rajani, Mkuu wa Twaweza, alisema, “kama ni kuifuta au kuiacha iendelee, uamuzi wa tozo ya Kodi ya SIM lazima utafakariwe kwa kina. Mjadala wa umma na tathmini ya matumizi ya watu ya simu ni jambo la muhimu la kufikiria. Ukizingatia vipato vya wananchi, ingekuwa vyema zaidi kukusanya maoni ya umma huhusu kufaa kwa Kodi ya SIM kabla ya uamuzi huu.”

---- Mwisho ----

Kwa taarifa zaidi

Risha Chande

Meneja Mawasiliano, Twaweza

barua pepe: rchande@twaweza.org | t: (+255) (0) 656 657 559

Matini kwa Wahariri

- Muhtasari huu na data zake unapatikana katika tovuti hizi: www.twaweza.org, au www.twaweza.org/sauti
- Twaweza ni jitihada ya miaka kumi inayoamsha msukumo wa kiraia na ambayo inalenga kuleta mabadiliko makubwa katika Afrika ya Mashariki. Twaweza inaamini kwamba mabadiliko ya kudumu huhitaji msukumo unaoanzia chini, na inatafuta kukuza hali na kupanua fursa ambazo kwazo mamilioni ya watu wanaweza kupata taarifa na kufanya mabadiliko hayo yatokee katika jamii zao na hasa kwa kuziwajibisha serikali moja kwa moja.
- Unaweza kufuatilia kazi za Twaweza kupitia:

Tovuti: www.twaweza.org **Facebook:** Twaweza Tanzania **Twitter:** @Twaweza_NiSisi